https://dspace.org/

# Ujumbe Wa Amani; Katika Uchaguzi Wa 2022 Tukumbuke Peek, Pii, Pwa, Biyo Zote Ni L'eau (Maji)

**Karama, Mohamed**

**2022-07**
Research Gate
https://www.researchgate.net/publication/362304261

Downloaded from a DSpace repository. https://dspace.org/

ResearchGate

See discussions, stats, and author profiles for this publication at: https://www.researchgate.net/publication/362304261

# UJUMBE WA AMANI; KATIKA UCHAGUZI WA 2022 TUKUMBUKE PEEK, PII, PWA, BIYO ZOT$^{h}$E NI L'EAU (MAJI)

**Article** · July 2022

CITATIONS
0

READS
71

**2 authors**, including:



Mohamed Karama
University of Kabianga

**14** PUBLICATIONS **2** CITATIONS

SEE PROFILE

**Some of the authors of this publication are also working on these related projects:**

Project UCHAMBUZI WA UTENDI WA SIRI LI ASRARI View project

All content following this page was uploaded by Mohamed Karama on 28 July 2022.

The user has requested enhancement of the downloaded file.

<u>**UJUMBE WA AMANI**</u>

**KATIKA UCHAGUZI WA 2022 TUKUMBUKE PEEK, PII, PWA, BIYO ZOṮʰE NI L'EAU (MAJI)**

Katika masiku ya hivi karibuni mashirika ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali nchini Kenya yamezinruka na kuonya kuhusu barabara wanasiyasa wanayoṯaka kutupeleka huku wakivutiya mikao yao katika Uchaguzi Mkuu unaokuja baaḏa ya muḏa kiḏogo ṯu. Kwa vile kila mwamba ngoma huvutiya kwake, basi, ikawa kumsetʰa mwenziyo ni sawa. Mbiyu za mgambo zilipoanza kufikiriwa kulizwa, Serikali Kʰuu imekuja haraka na kwingiliya kati ili kuweka nidhamu isohaṯarisha amani ya nchi. Haṯuwa hii ya Serikali Kʰuu ni jambo la kupongezwa na kushukuriwa.

Kama wasemavo wazee wetu waṯukufu waloitumikiya nchi hii kwa moyo wao woṯʰe, kura ni wingu la kupitʰa na keshowe kuṯakucha. Naswaha ya neno letu ni kwamba makunri yoṯʰe yaangaliye twaṯoka wapi, tukoje hivi sasa, na kesho twaiṯaraji siku iwe njema vipi.

Tukiyangaliya usawa wa binaḏamu kimaumbo yao, sisi twasema katika mwingiliyano wa lugha zao, piya, hakuna ilo bora kuliko nyengine. Lugha zilizomo Kenya ni nyingi na kila moja ina jukumu la kwenreleza ushikamano na ufungamano ili shabaha na lengo letu liwe moja: kuinuwa Kenya kihali na kimali. AMANI BAINA YA JAMII ZETU IMO KATIKA KILA KITʰU kama tuṯakavoonesha hapa chini.

Mfano mmoja tulouchaguwa sisi kwangaziya mwingiliyano huu ni neno ṯukufu lenye kunasibishwa na uhai wa mwanaḏamu kokoṯʰe aliko ulimwenguni. Yasemwa maji ni uhai. Kila lugha katika ulimwengu lazima inalo neno hili la kimsingi katika hazina ya misamiyaṯi yake. Maneno:

| | | |
|---|---|---|
| peek | – | kiKalenjin |
| pii | – | kiJaluo |
| biyo | – | kiKushiti |
| pani | – | kiHinḏi |
| pwa | – | kiSwahili lahaja |
| maji | – | kiSwahili Sanifu |

yoṯʰe yamaanisha maa (kiArabu), l'eau (hutamkwa 'lu') (kiFaransa). Tukiyangaliya kwa makini maneno yoṯʰe yaliyoorodheshwa yana sauṯi /p/, /b/ na /m/. Twaweza kusema asili yao ni moja kwa kuwa zoṯʰe ni sauṯi za miḏomoni na yanamaanisha 'maji'.

Katika kiSwahili 'pwani' ni mgawanyiko wa mofimu mbili /pwa- + -ni/. /-ni/ ni kiyelezi cha mahali. Waswahili wa Mambasa husema "kwenra baharini" na Waamu hunena, "kwenra pwani" kwa maana ya 'kwenra kwenye yale maji'. Kwa hivo, /pwa-/ ina maana ya 'maji'. Hata Shihabudin Chiraghdin katika *Historia ya Kiswahili* (1977) amelitumiya neno hili 'pwaa' kwa maana ya 'mwambao'. Hali kadhalika, bingwa mmoja wa kiSwahili alitwambiya kuwa 'mluo' ni kiSwahili cha kale linalomaanisha 'mto', hivo basi, dhana ya

maji i palepale. Yaweza kuwa piya ‘mluwo’ ni ukopaji kutoka lugha za kiRumi (kiFaransa katika mfano hapo juu). Kuṯokana na mfanano huu lugha zetu zatwambiya nini? Tukaye tuṯafakari kuwa maingiliyano yetu ni ya ṯangu jadi haṯa lugha zetu piya zasema hivo.

Kwa mintarafu ya mshikamano wa maneno yetu, vilevile, mwenenro wetu katika jambo hili la Uchaguzi Mkuu 2022 liwe ni la amani, uṯangamano na upenḏo katika nchi yetu. Hapana shaka ṯarehe 10 Agosti juwa liṯakucha tuṯake tusiṯake; imani yetu kuṯapambauka katika mafungamano ya kheri. **KAMA YALIVYO MAJI NI UHAI NA AMANI NI VIVYO!**

Mohamed Karama & Alexander Rotich
University of Kabianga
Kericho, Kenya.

View publication stats